# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo fulani zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu vituo ya ukaguzi na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## KAMA AFISA WA KUTEKELEZA SHERIA AO AFISA WA UHAMIAJI ANAKUYA KWAKO KUNYUMBA

- Kama polisi ao afisa wa uhamiajianakuya kwako kunyumba,  hauna haja ya kufungula mulango isipokuwa kama anakuonyesha kibali cha upekuzi yenye inasainiwa na muamuzi.
  - Usifungule mulango. Zungumuza nabo ukiwa mu nyumba kupitia mulango yenye inafungiwa ao kupitia dirisha. Baambie, "Siitike muingie ndani."
  - Muambiye polisi ao afisa wa uhamiaji akuonyeshe kitambulisho yake ao beji kupitia dirishani ao ku tundu ya kuangalilia ya ku mulango.
  - Bakisema bako na kibali, ubaambiye baipitishe chini ya mulango ao baionyeshe kupitia dirisha.
  - Hakikisha anuani yenye iko ku kibali iko ya muzuri.
  - Ni baamuzi ba jimbo ao ba serikali ya shirikisho tu njo banaweza kusaini kibali ya upekuzi. Baamuzi ba uhamiaji habapashwi.
  - Kama hauna uhakika, muulize afisa ni muamuzi wa aina gani alisaini kibali. Ao ubalombe bakupatiya muda ya kuita mwanasheria ku siku.
- Kama habana kibali ya upekuzi, hauna haja ya kubaingiza munyumba. Baambie, "Siitike muingie munyumba." Unaweza pia kukatala kuzungumuza nabo.
- Usichanganye kibali ya kufunga mutu na kibali ya upekuzi.
  - Kibali ya upekuzi inaruhusu maafisa wa kutekeleza sheria kuingia mu nyumba yako na kuifanyia upekuzi.
  - Kibali ya kufunga mutu inaruhusu maafisa wa kutekeleza sheria kukuya kwako kunyumba kusudi bakufunge. Lakini haiwape ruhusa ya kupekua nyumba yako.
  - Amri ya kutoshwa mu inchi ao kufukuzwa mu inchi (kibali ya uhamiaji) haipatiye afisa haki ya kuingia mu nyumba yako.



# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

## KAMA AFISA WA KUTEKELEZA SHERIA AO AFISA WA UHAMIAJI ANAKUYA KWAKO KUNYUMBA



- Kama maafisa bako nakibali halali ya upekuzi na banafanya upekuzi mu nyumba yako:
  - Kama unaishi na batu benye habako banainchi ba Marekani, ni muzuri batoke mu nyumba haraka na bafunge mulango nyuma yako. Hii inaweza kusaidia kulinda batu bengine benye banaishi mu nyumba zidi ya kuulizwa maswali ao kufungiwa na ICE.
  - Wakati upekuzi iko inafanyika, uko na haki ya kubakiya kimya. Sema, "Sipendi kujibiya maswali yenu."
  - Uko na haki ya kukuwa na mwanasheria, na kama unashukiwa kufanya uhalifu, polisi inapashwa kukupatia mwanasheria. Sema, "Minapenda nikuwe na mwanasheria."
  - Usizuwiye maafisa ao kubakataliya basiingiye fasi zenye ziliorozeshwa ku kibali.
  - Usiseme bongo wala kupana barua za bongo.
  - Usisaini kitu ata moya na hauya zungumuza na mwanasheria.
- Bakilazimisha kuingia, usibapinge kwa kinguvu. Sema, "Siitike kuingia yenu wala kufanya upekuzi mu hii nyumba." Minatumia haki yangu ya kubakiya kimya. Minapenda nizungumuze na mwanasheria.
  - Kumbuka muzuri byenye bilitokea moya kwa moya, na ukipata nafasi, kamata picha ao video.
- Lomba ukuwe na mutafsiri kama Kingereza haiko luga yenye unajisikia muzuri zaidi kuongea.

